YALIYOMO

1. **Ramani ya Parokia** ii
2. **Picha ya Paroko Mwanzilishi** iii
3. **Salamu za Askofu Mkuu wa Jimbo** iv
4. **Utangulizi** v
5. **Dibaji** vi
6. **SURA**

I. **Parokia ilivyoanza** 1

II. **Historia ya Uongozi** 8

III. **Juhudi za waamini na wafadhili** 12

IV. **Jumuiya ndogondogo katika Parokia** 15

V. **Vyama vya Kitume** 25

VI. **Nyumba ya Furaha na Amani** 46

7. **Matukio muhimu** 65

SURA YA KWANZA

PAROKIA ILIVYOANZISHWA

I. Hatua za Mwanzo

Mnamo miaka ya 60 wakristo wa maeneo ya Mburahati walikuwa wanahudumiwa Kiroho na Kanisa la Msimbazi ambayo ndiyo iliyokuwa Parokia Mama na Msimamizi wa Kituo cha Mburahati. Huduma hizo zilikwisha mwaka 1968 kutokana na sababu za Kijografia ambazo zilifanya kigango hicho kuwa chini ya Parokia ya Magomeni.

Wakati huo huo katika hatua za awali Kigango hicho kilisimamiwa na Padre Oswin Baumann Paroko wa Magomeni akisaidiwa na Padre John Manez aliyekuwa Paroko msaidizi.

Kutokana na maeneo hayo kuwa kama mashambani watu wengi walikuwa hawajabatizwa (wapagani) na wengi wao walikuwa ni kabila la Wamakonde. Mpango huo maalum wa kuwafundisha watu hao ulibuniwa na ulikuwa ukiongozwa na **LEGIO MARIA** waliokuwa wanatoka Magomeni na Mburahati. Padre Oswin alikuwa anawasimamia **WALEGIO MARIA** hao waanzilishi na walimu wa dini:

a. Mama Anastazia Adrian Kutoka Mgomeni
b. Mama Alfonsa Mselewa Kutoka Mburahati
c. Mama Maria Kasonya Kutoka Mburahati

Mama Anastazia Adrian alipata kiwanja cha shughuli hiyo katika eneo la Mburahati, sehemu ambayo sasa ni Hospitali ya **BAKWATA** katika barabara ya Mianzini inayounganisha Mburahati na Magomeni.

Katika kuunga mkono juhudi hizo Padre Oswin alichangia mabati, misumari na mbao na kazi za ujenzi wa banda la mafundisho zilifanywa na wakatekumeni hao kwa njia ya kujitolea.

Baada ya banda hilo kuisha Padre Oswin alikuwa anakutana na wana kigango hapo kwa kusali na kufanya mikutano mingine ya kidini.

Katika kuonyesha maendeleo ya kiroho kwa kigango cha Mburahati mwaka 1969 Padre Oswin alimteua Mama Alfonsa Mselewa kuwa mjumbe wa Halmashauri ya Parokia huko Magomeni.

Msukumo huo wa aina yake uliokuwepo kwa nguvu za Mungu hadi kufikia 06/03/1972 kamati ya Jimbo iitwayo **DEVELOPMENT OF RESOURCES** ilikutana na kukubaliana na kupanga nyumba ya utawa wa Tatu iliyoko maeneo Mburahati kwa shebe mtaa wa Makurumla **"A".** Nambari ya nyumba ni **AA 66** na wamiliki wa nyumba hiyo ni Utawa wa Tatu ulioko chini ya **MT.FRANCIS** wa Asizi.

Shughuli maalum ya nyumba hiyo ilikuwa kituo cha Ibada na Misa ambacho kilitumika hadi ilipopatikana Kanisa la Mburahati

Mnamo 02/07/1972 wakristo wa Mburahati waliazimisha Misa ya ufunguzi wa nyumba hiyo kama kanisa na misa hiyo ilihudhuriwa na wakristo wapatao 20-30. Mapadre waliokuwa wanasoma misa hapo ni

Padre Oswin na Padre John kutoka Magomeni, Padre J. Muba, Padre D. Mbiku, Padre Novatus kutoka Jimboni.

Pamoja na maendeleo ya mahudhurio ya waamini waliokuwa wanaendelea kuhudumia kiroho, mipango madhubuti ya kujenga kanisa dogo ulianza ambalo sasa linatumika kama ukumbi. Ujenzi huo ulichukua muda wa miaka mitatu (1972- 1974).

Baada kumalizika kwa nyumba hiyo iliyoko maeneo ya Mburahati NHC, kituo au kanisa ilihama kutoka nyumba ya ushirika wa Francis wa Asizi. Idadi ya waamini ilikuwa inaongezeka siku hadi siku.

Wanamburahati na Mapadre waliokuwa wanaongoza kanisa hilo walikuwa wanapambana na mawazo yao namna gani wapanue huduma hiyo iliyoendana na ongezeko la waamini. Mnamo 24/04/1974 kanisa dogo hilo lilianza kutumika rasmi.

Michango ya awali katika Misa na Ibada mbalimbali kanisani hapo ilikuwa kati ya 100/= na 200/=. Michango hiyo ya Ibada na Misa mbalimbali ilikuwa inachanganywa na michango mingine ambayo waamini wenye moyo walikuwa wanajitolea hasa wanalegio Maria ili kuzalisha tunda la parokia ya Mburahati

UZINDUZI RASMI WA PAROKIA YA MBURAHATI

Mbio hizo zilizaa matunda na 02/12/1974 Mburahati ilizinduliwa rasmi kama Parokia. Miongoni mwa waliozindua Parokia ya Mburahati ni Mwenyekiti wa Baraza la Walei wa Parokia ya Magomeni na Mtangazaji wa zamani wa Radio Tanzania ndugu Stephen Mlatie na Kamati yake.


II. MITAA YAUNDWA ILI KURAHISISHA KAZI YA UONGOZI WA PAROKIA

a. Uzinduzi huo ulimwezesha Padre Oswin Baumann kutoka Parokia ya Magomeni kuwa Paroko wa kwanza wa Parokia ya Mburahati. Kazi ya awali ya Paroko huyo ilikuwa ni kuhakikisha Parokia imegawanyika katika mitaa ili kurahisisha shughuli za uendeshaji. Mitaa 15 iliundwa kama ifuatavyo; Kwambera, Kilimahewa, Mianzini, Kwajongo, Mzambarauni, Minyonyoni, Mabibo A, Mabibo B, Kisiwani, NHC A, NHC B, Luhanga A, Luhanga B, Makurumla “A” na Makurumla “B”.

b. Kutoka kila mtaa waliteuliwa halmashauri wawili ili kusaidia Kamati ya Utendaji ya Parokia katika kuongoza Parokia. Padre Oswin aliishi Magomeni mpaka mwaka 1976 alipohamia rasmi katika nyumba yake mpya ya hapa Mburahati akitokea Magomeni. Ujenzi wa nyumba hiyo ili gharimu sh 75,000/=.

III. MBURAHATI WAMPONGEZA MAREHEMU CARDINAL LAURIAN RUGAMBWA KWA KUTIMIZA MIAKA 50

Mnamo tarehe 12/06/1977 waamini wa Parokia mpya ya Mburahati waliungana na wanajimbo wengine wakiongozwa na Baraza lao kumpongeza Kardinal Rugambwa alipotimiza miaka 50 tangu alipozaliwa. Sherehe ambayo iliadhimishwa katika Kanisa la Mtakatifu Joseph.



Kama kawaida wacha Mungu huwa mapumzikoni. Paroko mpya wa Mburahati alishindwa kuungana na wana parokia kwa kumpongeza Kardinal Rugambwa kwa kutimiza miaka 50 ili mwambata wake Padre Bruno alifanikisha sherehe hiyo kwa kiwango cha juu sana. Msaidizi wa karibu wa Paroko Oswin Padre Bruno alifariki tarehe 20/04/1994.

Wana Mburahati walishiriki kikamilifu msiba huo na sadaka yao ilikuwa Tshs. 480/=.

IV. UJENZI WA JENGO LA KANISA

Mwaka 1980 wana wa Mburahati waliungana na kupeleka nguvu zao katika mradi wa ujenzi wa Kanisa jipya pamoja na kuwa hali ya kifedha ilikuwa ngumu sana. Mwenendo wa ujenzi wa kanisa hilo ilikuwa wa kusuasua sana na ilichukua muda wa miaka miwili na kisha mambo ya ujenzi yalisimama. Hali hiyo iliwafanya Paroko, Mwenyekiti, Katibu na Mweka hazina kuchukua jukumu la kwenda kumuona Baba Askofu Kardinal Rugambwa (marehemu) na Padre Orsula ili kuwaomba msaada wa kuendeleza ujenzi huo.

Wana Mburahati hao walimtembelea Marehemu Baba Askofu huku wakiwa na michango toka kwa waamini. Kutokana na moyo wake wa huruma Kardinal Rugambwa alikubali maombi hayo na ujenzi huo kuanza tena mwanzoni mwa mwaka 1981.

Ujenzi huo ukiwa unaendelea mnamo mwezi August 1981 Padre Oswin alipata uhamisho kwenda Jimboni na nafasi yake ilichukuliwa na Padre Nesfori Maseko kama Paroko wa Mburahati. Mwaka huo huo Parokia ililetewa mwaliko wa sherehe ya upadrisho tarehe 22/11/1981 wa Padre **CAMILIUS LUAMBANO** ambaye familia yao ni waamini wa Mburahati.

Wazazi wa Padre Luambano walitoa ombi rasmi kwa Paroko wa Mburahati ili misa ya kwanza ya shukrani ya mtoto wao Padre Camilius Luambano isomwe ndani ya jengo lisiloisha la kanisa kama sadaka na changamoto ya kuomba Baraka kwa Mungu ili ujenzi wa kanisa hilo uende haraka. Misa ilifanyika mnamo tarehe 29/11/1981 kama walivyoomba.

Januari, 1982 Padre Maseko alikwenda mapumziko na mwana wa Mburahati na mtoto wa Jimbo la Dar es salaam Padre Camilius Luambano aliletwa kuchukua nafasi yake kama Paroko wa muda.

V. KUBARIKIWA/ KUFUNGULIWA RASMI KWA JENGO JIPYA LA KANISALA MBURAHATI NA MWADHAMA KARDINAL LAURIANI RUGAMBWA 20/04/1983

Ufunguzi huo ni pamoja na kulitamka rasmi jina la Parokia hiyo ambalo ni **KANISA KATOLIKI LA FAMILIA TAKATIFU MBURAHATI** mbunifu wa jina hili alikuwa Mama Adelaida Lyafwila.

Baada ya ufunguzi huo rasmi Mwadhama Kardinal Rugambwa alitoa Sakramenti ya Kipaimara kwa waamini wapatao **296**. Pamoja na furaha nyinginezo wanamburahati walitambua gharama za ujenzi wa kanisa hilo ni Sh. **2,200,000/=** (milioni mbili na laki mbili tu) wakati huo.

HIJA MAALUM

Vyama vya kitume Mburahati havikua nyuma mnamo 14/08/1983 waliungana wa waamini wa Parokia mbalimbali Jimboni Dar es salaam kwa hija maalum iliyofanyika Parokia ya Msimbazi.

MBURAHATI YAMPONGEZA KARDINAL RUGAMBWA KUTIMIZA MIAKA 40 YA UPADRE

Wana Mburahati bado walikuwa changamoto na chachu ya Jimbo kuu la Dar es salaam kutokana na kuungana na Parokia kongwe katika shughuli za kiroho ikiwemo sherehe ya kumpongeza Mwadhama Kardinal Lauriani Rugambwa alipoadhimisha miaka 40 ya Upadre zilizofanyika katika Kanisa kuu la Jimbo la Mtakatifu Joseph (cathedral Church) 29/01/1984. Kutokana na wingi wa waamini waliojitokeza Parokia ililazimika kukodi gari aina ya “Pick-up”

VI. MIPANGO NA UTEKELEZAJI BAADA YA UCHAGUZI WA PAROKIA

Baada ya Uchaguzi wa Viongozi wa Baraza Mwaka 1984

Mambo muhimu yaliyowachanganya vichwa viongozi waliochaguliwa ni pamoja na kutayarisha sherehe ya kutimiza miaka kumi ya Parokia ya Mburahati 30/10/1985 yaani 1975-1985 pamoja na shukrani za Mungu. Baraza liliwaalika watu toka mahali kwingineko Jimboni na Parokia jirani. Katika tafrija hiyo watu mbalimbali walizawadiwa kutokana na michango yao waliyoitoa tangu kuanzishwa kigango hadi Parokia na mgeni rasmi wa hafla hiyo alikuwa Paroko mwanzilishi Padre Oswin Baumann.

Katika mwaka 1987-1982 kulikuwa na mipango kabambe ya maendeleo ya Parokia. Miradi iliyopangwa kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

a) Ujenzi wa wigo (fence)
b) Ujenzi wa sehemu ya Sanamu ya Bikira Maria (Grotto)
c) Ununuzi wa vipaza sauti

Tarehe 10/10/1987 Parokia iliadhimisha Misa ya Shukrani ya Padre A. Lipingu (marehemu) kwa maandamano makubwa. Baada ya Misa ilifanyika sherehe ya kumpongeza Padre mpya ambaye alikuwa wa shirika la wakonsolata Padre DR. ALEXIUS LIPINGU (IMC)

Baada ya Uchaguzi wa viongozi wa Mwaka 1992 Baraza la Parokia liliazimia kufanya yafuatayo:-

- Kufanikisha mipango ya Misa maalum za kanda ambako ni kanda I na I.I
- Upanuzi wa ukumbi wa Mtakatifu Thomas
- Ujenzi wa Ofisi za Baraza la Walei/ Katekista
- Kusimamia Muungano wa vyama vya kitume 1993
- Ununuzi wa "Generator" ya umeme

Katika kipindi cha miaka 1995-1998 viongozi waliochaguliwa walikuwa na mtazamo wa kuivusha Parokia ya Mburahati toka katika kipindi cha matatizo sugu ambayo muda uliokwisha hayakutimia. Mambo hayo waliyoyatupia macho kwanza wakati wa kipindi chao cha uongozi ni:-

- Ujenzi wa barabara ya Mburahati
- Ujenzi wa stoo na huduma za choo
- Ununuzi wa generator mpya
- Ujenzi wa kisima cha maji

Baada ya uchaguzi wa mwaka 1998 Kamati ya utendaji iliyoundwa ilianza kufanya yafuatayo katika kipindi chake cha uongozi kati ya 1998-2001

- Kupaka upya rangi ndani na nje ya Kanisa
- Kufanya sensa ya waamini wote wa Parokia
- Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya mapadre
- Kununua gari la parokia
- Kuweka alama za kudumu makaburini ili kuwezesha usafi ufanyike vizuri
- Kuimarisha uongozi na uendeshaji wa JNNK
- Kufanya sherehe za Jubilei ya miaka 25 ya Parokia

Wakati kitabu hiki kinatayarishwa asilimia kubwa ya malengo hayo yalikwisha tekelezwa

SURA YA PILI

HISTORIA YA UONGOZI WA PAROKIA

PAROKIA YA FAMILIA TAKATIFU – MBURAHATI

Parokia ilizinduliwa rasmi kama Parokia ya Mburahati tarehe 2/12/1974. Mnamo mwaka 1975 Parokia iliunda uongozi wa Baraza kwa mara ya kwanza kwa mujibu wa katiba ya Baraza la Walei. Uongozi huo ulikuwa kama ifuatavyo:-

1975-1978

Paroko	- Fr. Oswin Baumann
Mwenyekiti	- Clemence Boniface
Makamu mwenyekiti	- Cosmas Mlinga
Katibu	- Martin Ndimbusha
Katibu Msaidizi	- Justine Theobard
Mtunza Hazina	- Marry Kasonya

Katika kipindi cha miezi 6 Ndugu Clemence Boniface alijiuzulu. Ndugu Cosmas Mlinga akateuliwa badala yake na Ndugu O. Ndunguru akawa Makamu Mwenyekiti.

Wakati huo Halmashauri ya Parokia iliundwa na wajumbe wawili kutoka kila mtaa, ambapo kulikuwa na mitaa kumi na tano iliyokuwa imeanzishwa katika kipindi hiki cha miaka mitatu.

Kwa mujibu wa katiba ya baraza la waleu baada ya kiupindi cha miaka mitatu viongozi wapya walichaguliwa uchaguzi huo ulileta viongozi wafuatao:-

1978-1981

Mwenyekiti	- Cosmas Mlinga
Makamu mwenyekiti	- Joseph Kingwale
Katibu	- Dickson Marandu
Katibu msaidizi	- John Haule
Mtunza hazina	- Marry Kasonya

Halmashauri iliendelea kuwakilishwa na viongozi wawili kutoka kila mtaa uongozi huo uliendelea kuongozwa na Paroko Oswin Baumann. Baada ya miaka mitatu kadiri ya katiba, uchaguzi wa parokia ulifanyika na viongozi wafuatao waliwekwa madarakani:-

1981-1984

Paroko	- Padre Nesfori Maseko
Mwenyekiti	- Cosmas Mlinga
Makamu mwenyekiti	- Kalista Ruambo
Katibu	- Goreth makukula
Katibu msaidizi	- Adelaida Lyafila
Mtunza hazina	- Marry Kasonya

Muundo wa baraza la Parokia kuwa na viongozi 5 kutoka kila mtaa ulianza rasmi kutumika. Uongozi huu pia ulidumu kwa muda wa miaka mitatu na viongozi wapya walichaguliwa na kamti tendaji ikawa kama ifuatvyo:-

1984-1987

Paroko	- Leonis Laugeverd
Mwenyekiti	- Cosmas Mlinga
Makamu mwenyekiti	- Kalista Ruambo
Katibu	- Goreth Makukula
Katibu msaidizi	- Pelagia Msaki
Mtunza hazina	- Marry Kasonya

Utaratibu wa kuwa na wajumbe wa kuteuliwa katika kamati ya utendaji ulianza rasmi na wajumbe wawili waliteuliwa kusaidia kamati tendaji ya parokia nao ni Odilo Kahyarara na Edwin Kachenje.

Katika kipindi hicho ndugu Goreth Makukula katibu wa parokia alihamia songea na ndugu John Haule alichukua nafasi hiyo ambapo naye aliacha uongozi na ndugu O. Kahyarara aliteuliwa kuichukua nafasi hiyo. Mwishoni mwa mwaka 1986 Paroko alirudi kwao uholanzi kwa matibabu na mwezi julai 1986 Padre **WOLFRAM** aliteuliwa na Askofu kuwa Paroko wa Mburahati, baada ya mwaka mmoja wa uteuzi huo Padre huyo alihamishwa na nafasi yake kuchukuliwa na Padre **CAMILIUS LUAMBANO** 5/09/1987.

Wakati huo huo Padre Walfaram aliteuliwa kuwa Paroko wa Mburahati kuanzia Julai 1986- Septemba 1987. Uongozi mpya ulichaguliwa kwa mujibu wa katiba ya baraza uchaguzi huo uliwaweka madarakani viongozi wafuatao:-

1987-1991

Paroko	- Camilius Luambano
Mwenyekiti	- Odilo Kahyarara
Makamu mwenyekiti	- Kalista Ruambo
Katibu	- Gabriel Mboya
Katibu msaidizi	- Pelagia Msaki
Mtunza hazina	- Simon Sizinga

Wajumbe wa kuteuliwa; Mama Edisa Mgweno na C. Mahona

Viongozi wapya walichaguliwa na ikaundwa kamati ya utendaji kama ifuatavyo:-

1991-1995

Paroko	- Camilius Luambano
Mwenyekiti	- Stephen Luambano
Makamu mwenyekiti	- Edisa Mgweno
Katibu	- Emmanuel Tibaijuka
Katibu msaidizi	- Pelagia Msaki
Mtunza hazina	- Stanslaus Masamba

Wajumbe wa kuteuliwa ni: Aloyce Mdime na Efrem Mushi

Baraza liliendelea kuwakilishwa na wajumbe watano kutoka kila mtaa (wajumbe wa kuteuliwa:-)

Mtunza hazina Ndugu Masamba alihama na Ndugu Charles Dolongo aliteuliwa kuwa Mtunza hazina. Kwa mujibu wa katiba uongozi mpya ulichaguliwa katika mwaka 1995. Uongozi huo wa kamati ya utendaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

1995-1998

Paroko - Camilius Luambano

Mwenyekiti - Stephen Luambano

Makamu mwenyekiti - Edisa Mgweno

Katibu - Sigsbert Shimbe

Katibu msaidizi - Gabriel Mboya

Mtunza hazina - Martin Matemu

Wajumbe wa kuteuliwa walikuwa ni: Aloyce Mdime na Efrem Mushi

Aliteuliwa Paroko Msaidizi Padre Andrea Mwekibindu katika kipindi hiki. Alipohamishwa, Paroko msaidizi mwingine Padre Paulo Njoka aliteuliwa ambaye naye alihamishwa kabla ya kipindi hiki kuisha.

Ulipofanyika uchaguzi wa Halmashauri ya Walei mwaka 1998 wafuatao waliunda kamati ya utendaji ya Parokia.

1998-2001

Paroko - Camilius Luambano

Mwenyekiti - Bruno Hinju

Makamu mwenyekiti - Almena Kapinga

Katibu - Pastory Masomhe

Katibu msaidizi - Cassian Njowoka

Mtunza hazina - Augustine hilemba

Mjumbe - Aloyce Mdime

Mjumbe - Edmund Mlelwa

Mjumbe - Odilo Kahyarara

Mjumbe - Elizabeth Nditegeyeko

Mjumbe - Albina Mnogasi

Baada ya muda katibu msaidizi ndugu Cassian Njowoka alijiuzuru na nafasi yake ikajazwa na ndugu Aloyce Mdime. Mwaka 1999 baada ya kufariki ndugu Almena Kapinga, ndugu Adelgiza Kasisi alichaguliwa kuwa makamu mwenyekiti na ndugu Fulgence Sallangi aliteuliwa kuwa mjumbe badala ya ndugu Aloyce Mdime. Kilipoanzishwa kigango cha Luhanga mwishoni mwa mwaka 2000 mwenyekiti ndugu Bruno Hinju na wajumbe ndugu Elizabeth Nditegeyeko na ndugu Fulgence Sallangi walihama,

nafasi hii ya mwenyekiti ilishikiriwa kwa muda na ndugu Odilo Kahyarara hadi uchaguzi wa mwezi wa saba 2001.

SURA YA TATU

JUHUDI ZA WAAMINI NA WAFADHILI KATIKA KUJENGA PAROKIA

I. JUHUDI ZA WAAMINI

Tangu mwanzo waamini wa Mburahati wamejijengea tabia ya kujitoa nafsi zao kwa ajili ya maendeleo ya Kanisa. Asilimia kubwa kwa kazi zilizofanywa kwa ujenzi, ukarabati wa majengo. Usafi wa Kanisa na mazingira yake, mapambo ya kanisani, mafundisho ya dini, matunzo ya Paroko, utoaji wa huduma kwa wasiojiweza, ulinzi na utunzaji wa mali ya Parokia kwa kipindi cha miaka 25 iliyopita, zimefanyika kwa nguvu za waamini kwa kujitolea.

Ifuatayo ni mifano halisi inayoonyesha jinsi nguvu za waamini zilivyookoa fedha nyingi ambazo zingetumika kufanikisha kazi iliyokuwepo

a. Kwa kuona umuhimu wa Paroko kuwa na chombo cha usafiri mapema kabla ya mwaka 1980 waamini walichanga na kununua gari kwa ajili ya Paroko. Gari hilo lilipochakaa lilibadilishwa kwa kununua gari jingine jipya ambalo Paroko analitumia mpaka sasa.

b. Katika ujenzi wa Kanisa waamini waliombwa na wakatoa michango ya fedha kwa ujenzi. Ingawa fedha waliyotoa ilikua kidogo lakini kiasi hicho kilikua ni kichocheo kwa wafadhili wa nje kutoa msaada wao hadi kulikamilisha jengo la Kanisa mwaka 1983. Ilipofika hatua ya kuweka mabenchi Kanisani michango ilitolewa na waamini. Mchango wa pili katika ibada za Jumapili ulianzishwa kwa madhumuni hayo na unaendelea mpaka sasa.

c. Mwaka 1988, Padre Leonius alipotuletea wavu wa kutengenezea wigo kuzunguka eneo la Kanisa, waamini mafundi na wasio mafundi walijitolea kujenga wigo huo. Walichimba msingi na wakamimina zege, wakasimika nguzo za chuma na kuzungusha wavu huo eneo zima. Geti la chuma ambalo ni imara na linatumika mpaka sasa na vijana mafundi wa Parokia yeu kwa kujitolea.


d. Mwaka 1989 waya wa wigo ulibadilishwa kwa ukuta wa matofali ya block ambayo yalifyatuliwa na wanaparokia vijana. Sehemu ya ukuta wa mbele ilikamilishwa kwa vyuma ambayo vilitayarishwa na kusimikwa na vijana wetu.


e. Mwaka 1998 Kanisa na ukumbi vilipakwa rangi kwa fedha zilizochangwa na waamini.

f. Mafundi wa kulipwa malipo ya kujitolea wakishirikiana na vijana walijenga grotto, na kijiduka cha Parokia.

g. Kati ya mwaka 1994 mpaka 2001 waamini wameendela kutoa michango ya fedha, vifaa na nguvu kazi kwa ajili ya nyumba ya mapadre. Kiasi cha karibu sh. Milioni 7,000,000/= zimechangwa na waamini. Mbali ya hiyo mafundi ambao wanaendelea kukamilisha

ujenzi ni wanaparokia hii, wanafanya kazi kwa malipo ya kujitolea wakisaidiana na VIWAWA





h. Waamini binafsi, au kwa pamoja katika jumuiya zao wamenunua na kutoa vifaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Kanisa kwa mfano, matololi, majembe, reki, feni za ukutani, viti, stuli, mikeka ya kupangusia miguu, zuria, mashuka ya Altareni, simu yam domo n.k.

i. Kiasi kikubwa cha matengenezo na ukarabati wa majengo, mabenchi, viti, taa za umeme, vipaza sauti na genereta yamefanyika kwa njia ya kujitolea waamini mafundi.

j. Kila Jumatatu na Jumamosi waamini kwa zamu huja Parokiani kufagia ndani na nje ya Kanisa na ukumbi; kusafisha vyoo, na wakati mwingine kupiga deki Kanisani na ukumbini, kufyeka majani katika mazingira ya kanisa. Bila kufanya hivyo wangeajiriwa wafanyakazi wa kulipwa siyo chini ya sh. 60,000/= kila mwezi au sh. 7,200,000/= kwa mwaka.

Bado waamini wanao moyo wa kuitegemeza Parokia yao kadhalika kulitegemeza jimbo kwa kutoa michango kadiri ya maagizo uya ofisi ya Askofu.

II. <u>WAFADHILI</u>

Kiasi kikubwa cha fedha kilichotumika kujenga ukumbi, ofisi, Kanisa, nyumba ya zamani ya mapadre kimetolewa na wafadhili wa nje. Kadhalika ni kwa misaada ya wfadhili hao tumepata vinanda, vipaza sauti na taberinakulo.

Tulipata misaada hiyo kutoka kwa marafiki na jamaa na waliowahi kuwa maparoko wetu; Fr. Oswin, Fr. Leonius na Fr. Luambano; wanakumbukwa kwa juhudi walizozifanya katika suala hili.

Kumekuwa na wafadhili wa hapa nchini pia waliotoa misaada yao mikubwa kwa maendeleo ya Parokia yetu. Bwana mmoja alitoa zuria jekundu kwa sehemu ya Altare, mwingine alitoa fedha kuudisha simu yam domo iliyokuwa imeketwa kwa muda mrefu. Wengine wametoa wavu kuzuia kunguru wasiingie Kanisani.

Mungu anajua jinsi ya kuwalipa wafadhili hao.

SURA YA NNE
JUMUIYA NDOGONDOGO ZA KIKRISTU

MWANZO

Katika Parokia yetu jumuiya ndogondogo zilianzishwa mwaka 1982 baada ya kamati ya kitaifa chini ya Mwenyekiti wa Idara ya Utume wa Walei Mhashamu Askofu Christopher Mwoleka kuweka misingi ya uaznishaji wa Jumuiya ndogondogo za kikristu nchini Tanzania mwaka 1976.

Jumuiya ya kwanza iliitwa Betlehemu ilizinduliwa katika Mtaa wa Luhanga “A” chini ya Mwenyekiti wake mzee Edwin Kachenje na Katibu wake ndugu John Haule. Wakishirikiana wawili ndugu John Haule na Bibi Maria Kachenje walianza kuzunguka katika Mtaa mzima wa Luhanga “A” na kuhesabu nyumba za wakatoliki. Mzee Joseph Michael wakati mwingine alisaidia kuzitambua baadhi ya nyumba. Zilipatikana nyumba 72. Walizipanga nyumba hizo katika jumuiya na kila moja ikiwa na nyumba 12. Himizo Kubwa kwa kila jumuiya ilikua ni kusali pamoja na kutafakari Injili.

Waliunda kamati mbalimbali za kushughulikia masuala ya mazishi, akina mama, vijana, uchumi na usuluhishi wa ndoa. Baadaye ndugu John Haule aliombwa kusaidia shughuli za uanzishaji wa Jumuiya katika mitaa mingine ya Parokia.

Pole pole jumuiya nyingine ziliendelea kuanzishwa katika Mitaa mingine ya Parokia.

Kila Jumuiya iliyoanzishwa ilipewa jina lake. Mwanzoni siyo jumuiya zote zilizojulikana kwa majina ya watakatifu kama ilivyo sasa. Kwa mfano katika Mtaa wa Luhanga “A” jumuiya zilipewa majina ya miji ya nchi Takatifu kama Betlehemu, Betania, Yerusalemu, Yeriko, Galilea na Nazarethi. Katika Mtaa wa Kwajongo jumuiya zilizoanzishwa mwaka 1982 zilijulikana kwa nambari tu, jumuiya namba 1, namba 2, namba 3,.

Haikuwa rahisi kuanzisha jumuiya kwa sababu madhumuni yake na jinsi ya kuanzishwa na kuziendesha havikueleweka kwa waamini wengi. Kadhalika kulikuwa na ugumu wa kuwapata watu wa kuongoza vyombo hivyo. Kw upande mwingine hapakuwa na mwongozo wazi, kutoka Parokiani au Jimboni kuhusu jinsi gani zianzishwe na ziendeshwe hizo jumuiya ndogondogo. Hivyo kwa kipindi cha miaka mittano ya mwanzo jumuiiya aetu zilianzishwa na kuendeshwa kwa mitindo iliyoigwa kutoka majimbo ya Songea na Rulenge.

SEMINA NA MWONGOZO JUU YA JUMUIYA

Ili kufanya masuala ya jumuiya ndogondogo yaeleweke kwa wanaparokia na yapate misingi imara ya kuyaendeleza mwaka 1985 Parokia iliandaa semina kwa viongozi wa Parokia na Mitaa juu ya jumuiya ndogondogo. Semina hiyo iliendeshwa na Padre Edmund kwa siku mbili tarehe 20-22/11/1985. Katika semina hiyo washiriki walipewa maelezo juu ya mada zifuatazo.

- Maana ya Jumuiya ndogondogo
- Nguzo za maisha ya kijumuiya
- Taratibu za kuendesha mikutano ya jumuiya
- Madaraka ya jumuiya
- Wajibu wa viongozi wa jumuiya

Baada ya semina hiyo kasi ya ufunguzi wa jumuiya mpya iliongezeka na hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 1987 jumuiya tayari zilianzishwa katika mitaa. Idadi ilikuwa imeongezeka mwaka hadi mwaka manwaka 1995 idadi ya jumuiya ilifikia 85 na mwaka 2000 jumuiya zilifikia 90 katika mitaa yote 17.

Mnamo mwaka 1985 kamati ya utendaji ya Parokia ilitoa waraka kwa mitaa yote kuelekeza mambo ya kuzingatia katika kuanzisha na kuendesha jumuiya ndogondogo katika Parokia. Mambo muhimu yafuatayo yalitajwa katika waraka huo:-

1. Kwamba jumuiya ndogondogo ni kikanisa kidogo, ni mkusanyiko wa familia mbalimbali kuanzia familia 5 hadi 12 na pia ni umoja wa familia. Ukizingatia mpango wa Mungu juu ya binadamu kwamba tunapaswa kuwa pamoja na kupendana katika jumuiya zetu. Nanukuu "Mkipendana watu wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu" (Mathayo. 7:21).
2. Nguzo za maisha ya jumuiya zilizoorodheshwa nazo ni:-
    a. Kusali pamoja
    b. Kusoma na kutafakari Injili
    c. Kuishi kiushirika
    d. Kujitolea kwa ajili ya ndugu zetu.
        i. Wanajumuiya walielekezwa kutambua umuhimu wa kisali pamoja katika jumuiya na majumbani (Umoja wa sala katika familia). Viongozi walitakiwa kuwakumbusha waamini maana ya sala.
        ii. Katika kutafakari Injili kwa pamoja ilikuwa viongozi wawasaidie waamini kutambua mwito wao:-
            - Kila mtu baada ya kusikiliza Injili ajiulize swali "Naguswa na nini katika Injili" (achague kitu kimoja)
            - Baadaye kiongozi amwombe kila msikilizaji ashiriki katika mazungumzo kwa kutaja nini kilichomgusa (NB. Fikara ya Injili siyo majadiliano).
        iii. Kuishi ki-ushirika hasa kujenga umoja kwa kusaidiana kijumuiya
        iv. Kujitolea kwa ndugu zetu na kuwa tayari kutoa nafsi zetu kwa kuondoa shida za wenzetu na hivyo kutimiza amri kuu ya upendo.
3. Waraka ulieleza taratibu za mikutano ya jumuiya zizingatie yafuatayo:-
    a. Kuwe na kipindi cha maisha ambapo wanajumuiya husalimiana kujuliana hali na kila mmoja kuwa huru kuzungumza na wenzake. Ni wakati wa kuorodhesha waliohudhuria na kuwatambulisha wanajumuiya wapya.

b. Kufungua mkutano kwa sala inayoongozwa na kiongozi mmoja wa jumuiya nap engine kufuatiwa na wimbo.
c. Baada ya ufunguzi hufuata kusoma na kutafakari Injili (NB. kwa kawaida msomaji hutayarishwa mapema)
d. Tafakari ya Injili hufuatwa na kujadili mipango ya maendeleo ya Jumuiya:-
   i. Kwanza zitolewe ripoti za utekelezaji wa maazimio uyaliyopita
   ii. Pili yafikiriwe mambo mapya ya kuondoa matatizo au kuendeleza jumuiya.
e. Mwisho- kikao kifungwe kwa maombi ya kushirikishana. Watu wachache wanaweza kuchaguliwa kutoa maombi, kiongozi wa jumuiya akitangulia.
f. Muhimu: Mikutano isichukue zaidi ya saa moja na robo.


4. Jumuiya zina madaraka juu ya malezi ya watoto na juu ya wanajumuiya wenyewe na kila mwanajumuiya akiwa mfano bora katika maisha ya Kikristo.
5. Kila jumuiya inaweza kuwa na viongozi wafuatao:-
   MWENYEKITI, MAKAMU MWENYEKITI, KATIBU, KATIBU MSAIDIZI NA MWEKAHAZINA.
   - Viongozi wa jumuiya wachaguliwe chini ya usimamizi wa viongozi wa mtaa wao.
   - Kila kiongozi wa jumuiya awe na sifa anzopaswa kuwa nazo kiongozi wa mtaa kwa mujibu wa Katiba ya Baraza la Walei.
   - Muda wa kushika uongozi unategemea jinsi wanajumuiya watakavyoona inafaa. Lakini lazima kuwe na uchaguzi baada ya miaka mitatu kufuatana na Katiba mpya ya Halmashauri ya Walei ambayo inasema kiongozi asiongoze kwa zaidi ya miaka 9 mfululizo.
   - Baada ya uchaguzi iliagizwa viongozi kupewa semina juu ya kazi zao.
6. Viongozi wa jumuiya wana wajibu ufuatao
   a. Wajue mahali wanapoishi wanajumuiya
   b. Wawe na orodha kamili za wakristo katika jumuiya zao
   c. Wafahamu shida za wanajumuiya
   d. Wawaelekeze au kuwasaidia wanajumuiya kutatua shida zao za kiroho na nyinginezo.
7. Kila jumuiya inatakiwa iwe na kumbukumbu zifuatazo:-
   a. Daftari ya orodha ya wanajumuiya wote
   b. Daftari ya fedha
   c. Maazimio ya mikutano na utekelezaji wake
      - Katika baadhi ya mitaa waraka huo ulizingatiwa barabara na uendeshaji wa jumuiya haukuwa na matatizo mengi sana. Mpaka sasa asilimia Kubwa ya shughuli za uendeshaji wa jumuiya zetu nyingi unafuata waraka huo.

III. MAENDELEO BAADA YA KUUNDA JUMUIYA

Mara baada ya kuanzishwa jumuiya ndogondogo mabadiliko makubwa yameonekena miongoni mwa maisha ya wanaparokia na katika shughuli za uendeshaji wa Parokia kwa ujumla.

a. Waamini wengi wamefahamiana na kuendelea kuwa na hamu ya kufahamiana zaidi katika sehemu za makazi yao. Tabia kati ya baadhi ya waamini kuficha imani zao imefifia au kutoweka kabisa.

b. Wanashirikiana katika shida na raha mbalimbali kwa mfano wakati wa misiba, magonjwa, wakati wa sherehe za harusi, komunio ya kwanza na kipaimara. Mahali pengine waamini wameanzisha na kujenga vituo vya chekechea mfano:- Mt. Theresia, Mtaa wa Makutano



Picha ya kituo cha Makutano

c. Moyo wa kupendana umeongezeka hivyo waamini wengi kuwa katika hali ya kukumbuka mara kwa mara utimizaji wa Amri kuu ya Upendo “Mpende jirani yako kama nafsi yako”.
d. Kumekuwa na nafasi nzuri kwa kila muamini kuweza kuzungumzia masuala ya maendeleo ya Kanisa na kutoa maoni yake; pia kumekuwa na ongezeko la Demokrasia katika Kanisa.
e. Mawasiliano kati ya viongozi wa Parokia na kila muamini yamerahisishwa kutokana na kuwako kwa jumuiya. Paroko anaweza:-
    - Kuwafahamu waamini wengi na shida zao kwa urahisi.
    - Wenye shida wanatambulika haraka na wenzao na hivyo kusaidiwa kupata huduma kadiri inavyowezekana. Taarifa kutoka Parokiani zinawafikia wanajumuiya kwa haraka.
f. Kila muamini ana nafasi maridhawa ya kuweza kutumia karama zake kwa kulijenga na kuliendeleza kanisa kwa kupitia jumuiya wenye uwezo wa kuongoza, uwezo wa kuimba kuimba, wenye uwezo wa kutafakari Injili na kadhalika wana nafasi zaidi.
g. Uongozi wa Parokia na wa Mitaa umepata urahisi wa kuhimiza shughuli za kujitolea kwa kuliendeleza kanisa. Kadhalika ushirika wa waamini kwa shughuli zao hizo unaridhisha. Jumuiya zimerahisisha ukusanyaji wa michango mbalimbali kwa mfano michango ya ununuzi wa gari la parokia, kupaka rangi Kanisa, ujenzi wa nyumba ya mapadre, michango ya kulotegemeza Jimbo na ukusanyaji wa zaka.
h. Mahudhurio kwenye ibada za misa za jumapili yameongezeka na hivyo utoaji wa sadaka kuongezeka. Wakati wa kwenda kanisani baadhi huhimizana au kualikana kwenda pamoja. Vilevile wakristo wengi wamejitokeza kwa ajili ya kupata sakramenti mbalimbali.

Kila mwaka wanaparokia wameendelea kufaidi matunda hayo ya kuwa katika jumuiya na hivyo uhai wa Parokia kuendelea kuimarika.

IV. MISA KATIKA JUMUIYA

Mnamo mwaka 1987 Paroko Fr. Camilius Luambano alianzisha utaratibu wa kusoma misa katika Jumuiya. Hii imetoa nafasi kwa wanajumuiya kusherekea siku kuu za watakatifu wasimamizi wa jumuiya zao huko jumuiyani. Kadhalika imekuwa ni njia ya kuwajumuisha waamini katika makazi yao kwa lengo la kumtangaza Kristo kwa wenye imani tofauti na kuzidi kuwaimarisha wanaparokia katika imani yao.

Sambamba na misa hizo pia kulikuwa na matukio ya kubariki nyumba za walioomba kbla ya misa, kuungamisha wanaohitaji, kubatiza watoto katika ibada na mahali pengine kufungisha ndoa. Wakati wa mahubiri Paroko hupata nafasi ya kufafanua baadhi ya vipengele vya dini vinavyokuwa na utata nap engine kuzungumzia njia za kutatua matatizo yanayohusu hasa jumuiya inayohusika.

Katika Jumuiya nyingi baada ya misa waamini wana utamaduni wa kufanya sherehe na tafrija ya wanajumuiya wote watoto na watu wazima kwa nia ya kuwafanya wajuane, wale pamoja na hivyo kuimarisha na kudumisha upendo kati yao. Gharama za kufanikisha sherehe na tafija hizo ni juu ya wanajumuiya wenyewe. Kunakuwa na utaratibu wa kumsomea Paroko risala na wakati mwingine kutoa zawadi ama kwaajili ya Paroko mwenyewe, ama kwa wasiojiweza au kwa ajili ya maendeleo ya Parokia, mathalani;- viti vya ukumbi, vifaa vya ujenzi wa nyumba ya Padre na vifaa vya usafi wa kanisa na kadhalika.

Utaratibu wa kuadhimisha Misa katika jumuiya na Parokia zetu umeota mizizi na unaendelea. Kila mwaka Parokia inatayarisha kalenda ya kusoma Misa hizo huko mitaani/ waamini wengi wanapenda mpango huo na kujiandaa kwa misa hizo. Mwaka 1997 Mwashamu Askofu Pengo (kabla hajawa Kardinali) kwa kuunga mkono utaratibu wa Misa kusomewa nje ya makao makuu ya Parokia alikubali mwaliko na akaja kuadhimisha misa katika kanda mbili ziliunganisha waamini wa jumuiya majirani. Misa hizo zilisaidia kufanikisha kampeni ya ukusanyaji mchango wa Seminari ya Visiga.

V. MATATIZO YA UENDESHAJI

Kwa muda wote tangu jumuiya zianzishwe mwaka 1982 hadi leo kumekuwa na matatizo mbalimbali katika uendeshaji. Baadhi ya matatizo hayo ni:-

a. Siyo viongozi wote wamekuwa na sifa za kazi walizochaguliwa.

b. Baadhi yao wamebaini kutoelewa kazi na wajibu wao kadiri ya katiba ya Walei.

c. Mifano ya tabia mbaya miongoni mwa viongozi imewafanya mara nyingi washindwe kufanya vizuri kazi zao za kitume.

d. Karibu kila jumuiya mahudhurio ya wanaume kwa mikutano na sala za Jumuiya ni mabaya mno.

e. Nguzo Kubwa za jumuiya katika sehemu kadhaa zimeporomoka; hakuba sala za pamoja, hakuna tabia ya kusoma na kutafakari Injili na kadhalika.

f. Ni idadi ndogo ya jumuiya hutunza kumbukumbu zake vizuri.

g. Kwa waamini walio wengi maana halisi ya jumuiya ndogondogo za kikristo imechukua muda kueleweka.

h. Bado jumuiya zetu nyingi ni kubwa mno kiasi cha kufanya mawasiliano kati ya waamini wao kwa wao na viongozi kukwama.

i. Juhudi kubwa imefanywa na viongozi wa Parokia kwa njia ya mahubiri na semina mbalimbali kujaribu kutatua matatizo yaliyo orodheshwa hapo juu. Hii ni kuzingatia ukweli kwamba jumuiya ndogondogo ni msingi wa kanisa. Kadiri jumuiya zinavyoendelea kuwa bora ndivyo kanisa ki-mitaa, kiparokia, kijimbo, ki-Taifa na ki-ulimwengu mzima linavyozidi kuendelea kuwa bora.



Tarehe 11/2/2001 Sr. Maximilian kutoka Msimbazi aliendesha semina kwa viongozi wote ngazi ya Parokia, Mitaa na jumuiya kuhusu jinsi ya kuendesha jumuiya ndogondogo za Kikristo. Lengo lilikuwa ni kutatua matatizo yaliyotajwa hapo juu. Semina imefanikiwa na ni tegemeo letu kuwa jumuiya zetu sasa zitakuwa na sura mpya.

SURA YA TANO

VYAMA VYA KITUME

I. UTUME WA FATIMA

Historia ya Utume wa Fatima- Parokia ya Familia Takatifu- Mburahati 1989-2001

Hiki ni miongoni mwa vyama vya kitume ambacho kimeshamiri Mburahati. Utume wa Fatima Parokia ya Familia Takatifu Mburahati ulianzishwa mwaka 1989. Mwanzilishi wa Utume huo parokiani hapa ni sista Lysa aliyekuwa Mama Mkubwa wa shirika la Mama Tereza katika "convent" yao iliyoko hapa Mburahati, kisha ukaingizwa rasmi Parokiani kama chama cha kitume.

Sista Lysa alikuwa na nia ya kuanzisha utume huo toka mwaka 187 lakini hakufanikiwa kutokana na sababu mbalimbali hadi alipofanikiwa kumshirikisha Mama Kalista Ruambo ili amsaidie kufanikisha lengo hilo. Sists Lysa na aMama Kalista Ruambo kwa pamoja walimwendea Padre Camilius Ruambano na kumweleza nia na msimamo wao wa kuanznisha chama cha Utume wa Fatima. Naye Paroko alipeleka suala hilo kwa Askofu ili amweleze na ikiwezekana apewe kibali cha kuanzisha utume huo. Katika kugawana majukumu, Mama Ruambo alimfuata mwenyekiti wa Jimbo wa Utume wa Fatima ndugu Francis Mlowoka na kuongea naye ili kufahamu na kueleimishwa zaidi maana, madhumuni na masimamo wa chama hicho.

Masista wote wa nyumba ya masista hapo Mburahati alikubali kula kiapo kwa Mungu kupitia Mama Bikira Maria wa Fatima mwaka 1989. Baadaye walitafutwa wanachama walei wa Parokia ya Mburahati na wakapatikana wanachama 18 wanawake 17 na mwanaume 1 majina ya waanzilishi hao ni Kalista Ruambo, Maria Kasonya, Hyasintha Mapunda, Epifania Mapuinda, John Mahendeka, Clara Pagungire, Hildergard Luambo, Brighter Peter, Getrude Madohora, Josephine Mwambunga, Rainatha Msiwau, Albina Mnogasi, Sofia Zakaria, Cecilia Kins, Bibiana Peter.

Wanachama hao 18 walikula kiapo kuwa wanachama wa Utume wa Fatima kwa ibada maalum iliyoendeshwa na Padre Camilius Luambano tarehe 24/08/1989. Kwa muda usiopungua miezi mitatu wanachama hao walisali wakijifunza na kutafakari bila viongozi waliochaguliwa na kuwa chini ya sista- mwanzilishi Lysa aliendelea kuwaongoza na kuwatia moyo. Mwisho wa kipindi hicho cha mpito wanachama hao waliwateua viongozi wao kama ifuatavyo.

Uteuzi huo kwa mara ya kwanza ulifanyika mwaka 1989 na hao ndio walioitikia sauti ya Mungu

1. Ndugu John Mahendeka – Mwenyekiti
2. Mama Maria Kasonya – Makamu Mwenyekiti
3. Mama Hyasintha Mapunda – Katibu

4. Mama Getrude Madohora – Katibu Msaidizi
5. Mama Clara Pagugire – Mtunza hazina
6. Mama Kalista Ruambo – Promota/mwenezi

Kwa mujibu wa chama viongozi hao walipewa na kusomewa katia ambayo ilisomwa na kuzingatiwa malengo yote yaliyoamriwa. Pia wanachama wenyewe walijiwekea msimamo katika shughuli zao za kutaka kujifunza. Mwaka 1992 baada tu ya uchaguzi wa mwaka 1991 Mwenyekiti alipatwa na matatizo ya kiuendaji na kusimamishwa uongozi na Baba Paroko na nafasi hiyo ikajazwa na ndugu Pastory Masomhe. Mwaka 1995 ukafanyika uchaguzi wa viongozi kwa kufuata katiba amabo ni uchaguzi wa kwana wa chama hicho. Waliochaguliwa ni:-

1. Pastory Masomhe – Mwenyekiti
2. Maria Kasonya- Makamu mwenyekiti
3. Hyasintha Mapunda – Katibu
4. Charles Mkasi – Katibu Msaidizi
5. Clara Pagungire – Mtunza hazina
6. Kalista Ruambo – Promota
7. Cosmas Mlinga – Mshauri

Mfululizo wa chaguzi kikatibu zilichukua mkondo ake wa awamu nyingine ilikuwa mwaka 1998. Waliochaguliwa walikuwa.

1. Pastory Masomhe – Mwenyekiti
2. Kalista Ruambo – Makamu mwenyekiti
3. Hyasintha Mapunda – katibu
4. Leonard Sikale – Katibu msaidizi
5. Brighter Peter – Mtunza hazina
6. Cosmas Mlinga – Mshauri

Huu ndio mtiririko mzima wa chama cha Utume wa Fatima kuanzia mw aka 1989-2001.

- **Malengo ya chama cha Utume wa Fatima ni:-**

Kuishika ibada ya majitoleo kwa Mama Bikira Maria kwa kuvaa daima skapulari ya hudhurungi.

i) Kujitoa sadaka kwa kupokea yale yote tunayopewa na Mungu katika maisha yetu.
ii) Kusali mafungu matano ya rozari kila siku
iii) Kuwa na ibada ya saa Takatifu mbele ya Sakramenti kuu mara kwa mara

- Kazi zinazofanywa na Utume wa Fatima
  Kila Jumamosi kusali misa kwa nia zifuatazo:-
  - Kuwaombea wagonjwa
  - Kuwaombea wakosefu
  - Kuombea amani duniani
  - Kuwaombea marehemu waliosahauliwa toharani.

- ❖ Kila mwanachama anapaswa kusali mafungu matano ya rozari kwa nia hizo hapo juu kila siku katika maisha yake na kujiombea mwenyewe.
- ❖ Kuabudu Ekaristi Takatifu kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi na kuhudhuria ibada ya pamoja na kupokea Sakramenti. Pia kila jumamosi kusali kwenye grotto sala za utume.

Kazi hizo zifanywe na wanachama hao Mama Bikira Maria aliagiza zifanywe sio kwa matangazo ili kupata sifa bali kwa unyenyekevu na utii sirini.

Pia wanachama wanfanya shughuli zingine kama kufarijiana katika shida mbalimbali nakadhalika. Walezi wa chama cha Utume wa Fatima ni Masista wa Mama Tereza wa Parokia yetu.

II. WAWATA

Katika Parokia ya Mburahati WAWATA ilianzishwa tarehe 3/4/1975. Kiongozu wake wa kwanza alikuwa Mama Annaastazia Adrian ambaye alikuwa ni mwanaparokia ya Magomeni.

Baada ya muda kidogo wanachama waanzilishi wapatao 15 waliwachagua viongozi wafuatao

1. Maria Kasonya – Mwenyekiti
2. Teresia Ndunguru – Makamu mwenyekiti
3. Theresia Mavanda – Katibu
4. Filberta Ndunguru – Katibu Msaidizi
5. Justino Theobald – Mtunzahazima
6. Saveria Kahyarara – Mjumbe
7. Perazia Kaloli – Mjumbe

Hawa wwaliongoza chama hadi mwaka 1978 ulipofanyika uchaguzi mkuu wa viongozi wote wa Parokia.

Kati ya mwaka 1978-1981 kazi Kubwa iliyofanyika ni kuwahamasisha wakina mama kuendesha kazi za kuendeleza kanisa changa wakisaidiana na Padre katika usafi wa mazingira, kufagia ndani na nje ya kanisa. Katika kipindi hicho idadi ya wanachama iliongezeka kufikia 25.

Mwaka 1981 ulifanyika uchaguzi wa viongozi wa chama kwa kipindi cha miaka mitatu mwaka 1981-1981. Katika kipindi hicho wanachama waliongezeka kufikia 40. Mwaka 1982 WAWATA ilianzisha matawi yake katika kila Mtaa wa Parokia. Walichaguliwa viongozi watano akiwemo; mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi na Mtunza Hazina kwa kila Mtaa. Kadhalika kila Mtaa uliteua wajumbe 9. Katika zoezi hilo chama kilifanikiwa kuongeza idadi ya wanachama kufikia 180.

Baadhi ya WAWATA kusambaa mitaani shughuli zake ziliongezeka na idadi ya wanachama na watendaji ikawa inaongezeka kila mwaka. Mwaka 1984 wanachama walifikia 200.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 1987 hakukuwa na kiongozi mwanzilishi aliyebaki. Mama Maria Kasonya alikuwa kiongozi mwanzilishi wa mwisho kustaafu mwaka 1987. Hata hivyo kuondoka kwa viongozi hao waanzilishi hakukuathiri sana maendelelo ya chama.

B. KIPINDI KATI YA MWAKA 1987-2001

Kuanzia mwaka 1987 hadi mwaka 2001 kazi na shughuli zote za chama zimeendelea kama zilivyokuwa wakati wa uongozi wa waasisi hao kwa mfano:-

a. Uchaguzi wa viongozi kwa vipindi vyote vya miaka mitatu ulifanyika. (Vipindi 1987-1991, 1991-1995, 1995-1998, 1998-2001).
b. Kusafisha Kanisa, kusafisha makaburi, kufanya mikutano kwa mujibu wa Katiba, kufarijiana, kufanya mafungo, kupokea wageni, mfano Baba Askofu, kuandaa sherehe mbalimbali kwa mfano Mapadre wapya wanapokuja kusoma Misa za shukrani, kukaribisha au kuaga mapadre wanapoingia na kuonndoka.

Katika kipindi kuanzia 24/5/1997 hadi mwaka 2001 WAWATA imefanikiwa pia kufanya mambo tofauti na yale ya zamani kama ifuatavyo:-

1. Kila mwaka WAWATA Parokia huchangia shs. 15,000/= kama mchango wa kutunza na kulea seminari ya Visiga. Mchango huu huambatanishwa na michango mingine kutoka katika Parokia zote za Jimbo kuu la Dar es salaam. Baada ya michango yote kukusanywa kijimbo WAWATA woe hupeleka michango hiyo katika seminari ya Visiga. Michango hiyo huambatana na zawadi zingine mbalimbali kama madaftari, rula, kalamu, peni, sabuni, mafuta ya kupikia, mchele, unga n.k. WAWATA Parokia ya Mburahati wameshiriki kikamilifu kila mwaka katika kutoa michango, kutoa zawadi pamoja na safari ya kwenda kwenye shule ya seminari bila kukosa.
2. Shughuli ya pili ni Hija, hii mara nyingi huwaunganisha pamoja WAWATA wa sehemu zote za Jimbo. Hija nyingi hufanyika huko Pugu lakini mwaka Mtakatifu wa 2000 Hija hiyo ilifanyika Bagamoyo. WAWATA wapatao 60 kutoka Mburahati walishiriki kikamilifu.
3. Jambo jingine ni majitoleo ambayo hufanyika kwenye nyumba ya watoto yatima Mburahati, katika Nyumba ya Furaha na Amani kwa Mama Teresa. Majitoleo hayo hufanyika mara moja kwa mwezi kwa Mitaa miwili miwili ikishirikiana pamoja. Wakati wa siku kuu Kubwa hasa Noeli na Pasaka wakina mama wote hufanya majitoleo kama tendo la huruma ili kujiandaa kiroho na kuadhimisha siku kuu